*Unguja*
*09 Septemba, 2026*

Email: press@ikulu.go.tz

# TAARIFA KWA UMMA

## UJUMBE WA SHUKRANI KUTOKA KWA MHESHIMIWA DKT. SAMIA SULUHU HASSAN, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na familia yake, wameguswa sana na upendo, mshikamano, salamu za pole, dua na maombi waliyopokea kutoka ndani na nje ya nchi kufuatia kifo cha mume wake mpendwa, Bw. Hafidh Ameir Hassan, kilichotokea Zanzibar, tarehe 07 Septemba, 2026.

Katika kipindi hiki kigumu cha majonzi, Rais Dkt. Samia anatoa shukrani za dhati kwa Wakuu wa Nchi na Serikali, viongozi wa kitaifa, wanadiplomasia na jumuiya ya kimataifa, viongozi wa dini na Watanzania wote kwa salamu, dua na faraja zao katika kipindi chote cha majonzi, hadi leo wanapohitimisha siku tatu za maombolezo ya kuondokewa na mpendwa wao.

Bakari S. Machumu
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu